# Shule za Lugha ya-Kifaransa

# Karibuni Wanafunzi Wapya

## Je wewe ni mgeni Ontario? Hizi ni taarifa za kuweza kukusaidia kuelewa mfumo wa Kifaransa hapa Ontario.

### Kujifunza Kifaransa kunawanufaisha wanafunzi

Wanafunzi wana manufaa mengi zaidi wakizungumza lugha zaidi ya moja. Kujifunza lugha nyingine kunasaidia wanafunzi:

- kuimarisha mbinu zao za kutatua matatizo, kufikiria na kujenga ujuzi kwa njia ya ubunifu
- kuchochea uelewa na kukubaliana na mwingiliano wa tamaduni mbalimbali
- Kuongeza matazamio yao katika soko la ajira linaloongezeka duniani.

Kujifunza Kifaransa kunasaidia wanafunzi kuelewa historia ya Kanada na kuweza kuchochea utambuzi wa utamaduni wa Kifaransa.

### Namna ambavyo Kifaransa hufunzwa katika shule za Ontario

Ndani ya mfumo wa elimu unaofadhiliwa na umma wa Ontario , wanafunzi wanaweza kusoma kifaransa kama:

- lugha ya kwanza kupitia shule zinazofunza lugha ya kifaransa au
- lugha ya pili kupitia shule zinazofunza lugha ya kiingereza.

Katika shule za lugha ya Kifaransa, masomo yote katika lugha ya mtaala wa Ontario yanafunzwa kwa lugha ya Kifaransa. Shule zinatarajiwa kuweza kuwapatia wanafunzi wao msingi thabiti katika utamaduni wa Kifaransa. Katika shule za lugha ya-Kiingereza, wanafunzi hufunzwa Kifaransa kwa njia ya somo. Katika programu tumbukizi za Kifaransa, wanafunzi wanafunzwa Kifaransa katika lugha ya maelekezi kwenye masomo mengine mawili au zaidi.

### Nani anastahili kuhudhuria shule ya lugha ya-Kifaransa?

Hapa Ontario, ufikivu wa elimu ya lugha ya Kifaransa unahakikisha watoto ambao wazazi wao ni raia wa Kikanada na wanayo haki ya elimu ya lugha ya- walio wachache kuulingana na mkataba wa Haki na Uhuru. Wazazi hawa wanachukuliwa kuwa wanaostahili.

Mwenye haki ni raia wa Kanada ambaye:

- Anaishi Ontario na lugha yake ya kwanza ni kifaransa; au
- amepokea elimu yake katika kiwango cha msingi kwenye shule ya lugha ya-Kifaransa nchini Kanada :
- Ni mzazi wa mtoto ambaye amepokea elimu katika shule ya lugha ya-Kifaransa nchini Kanada.

Kama wewe si mwenye haki hizi, unaweza kutuma maombi ya kumpeleka mtoto wako katika shule za kifaransa. Shule za kifaransa zinahimiza maombi haya kutoka kwa familia zilizo ngeni hapa Ontario.

### Namna ya kutuma maombi katika shule ya lugha ya Kifaransa.

Ili kumpeleka mtoto wako kwenye shule ya lugha ya-Kifaransa, lazima:

- tambua shule za lugha ya kifaransa zinazotimiza ubora wa mahitaji yako
- wasilisha maombi yako kwa mkuu wa shule.

Kwa wanafunzi walio na umri wa miaka 19 au zaidi waweza kuwakilisha maombi peke yao. Wanafunzi ambao wazazi wao ni wenye haki hizo watachukuliwa moja kwa moja. Na wale wanafunzi ambao wazazi wao hawana haki hizo , maombi yao yatatakiwa kuzingatiwa na kamati ya bodi ya shule ya kuchukua wanafunzi.

Kama wewe si mwenye haki hizo, bodi ya shule inaweza kukuelezea namna ya kuwasilisha ombi na nyaraka zipi unazohitaji kuwasilisha. Hizi kwa kawaida hujumuisha:

- kithibitsho cha umri wa mtoto wako
- kithibitisho cha mtoto wako au wewe mbali mnaishi
- matokeo ya kitaaluma ya mtoto wako
- rekodi ya chanjo ya mtoto wako.

Kamati ya bodi ya shule ya kuchukua wanafunzi inaweza kuitaji taarifa za ziada. Kwa mfano; waweza kukuuliza hojaji kuhusu namna unavyotumia kifaransa nyumbani na lugha ambayo unaweza kuongea na kuandika.

Mfano ni wapi ambapo nyaraka hizo hazipatikani, bodi yako ya shule inaweza kukupatia njia mbadala. Bodi ya shule inaweza kukuuliza au mtoto wako (kama anaumri wa miaka 19 na zaidi) kuweza kuapishwa au taarifa ya kudhibitisha iliyoombwa na kufafanua kwa nini nyaraka hizi zimekosekana.

## Sera na mpangilio wa kuchukuliwa

Kila bodi ya shule ya lugha ya-Kifaransa huweka wazi sera zake za kuchukua wanafunzi ambazo zinaelezea kwa uwazi namna ambavyo maombi hushughulikiwa na namna ambavyo matokeo yataweza kuratibiwa na kuwasilishwa kwa wahusika. Mpangilio wa kuchukuliwa kwa wale wasio na haki hizo unalenga katika kutathmini uwezo wa kila familia katika kusaidia ufanisi wa mtoto wao katika mazingira ya shule ya lugha ya -Kifaransa. Mpangilio huu unaweza kujumuisha:

- kiwango cha ufasaha wa mwanafunzi katika Kifaransa
- Umakini wa mwanafunzi katika kujifunza Kifaransa
- Kujitolea kwa mzazi katika kusaidia maendeleo ya kitaaluma ya mwanafunzi katika Kifaransa.

## Namna ambavyo wazazi na wanafunzi watapata kujua kuhusu uamuzi wa shule

Kamati ya kuchukua wanafunzi inaweza kuwaambia waliotuma ombi kuhusu uamuzi wake, lakini thibitisho kwa maandishi lazima lifuate. Taarifa ya thibitisho hilo inafaa kuelezea sababu za uamuzi wao. Kamati ya kuchukua wanafunzi lazima iweze kuandika rekodi za uamuzi wake na kuhakikisha kwamba nyaraka zote zinazohusika zinafikishiwa wazazi na wanafunzi ili waweze kuhakiki. Baadhi ya bodi za shule zinaweza kuwa na mchakato wa kuhakiki uamuzi huo na mchakato huu wa uhakiki unafaa kuelezewa waziwazi katika sera zao.

## Namna ya kupata bodi ya shule ya lugha ya-Kifaransa

« L'Outil de recherche d'information sur les écoles » ni zana ya mtandaoni ambayo hukuruhusu kutafuta shule yoyote inayofadhiliwa kwa umma ukitumia msimbo wa posta, mji/jiji, jina la shule au bodi ya shule. Tafuta shule au bodi ya shule hapa Ontario katika: www.edu.gov.on.ca/fre/sbinfo/

Aidha, njia mbadala ni kuweza kutumia zana ya kitafutizi ya shule za lugha ya lugha-Kifaransa: www.elfontario.ca/fr/trouver-ecole.html inayopatikana katika tovuti ya elimu ya lugha ya-Kifaransa hapa Ontario: www.elfontario.ca/

## Jifunze zaidi kuhusu elimu ya lugha ya-Kifaransa

Soma zaidi kuhusu elimu ya lugha ya-Kifaransa hapo Ontario katika:
www.edu.gov.on.ca/fre/amenagement/

Soma maelezo zaidi kuhusu sera na miongozo inayotawala kuchukuliwa kwa wanafunzi katika shule za lugha ya-Kifaransa:
www.edu.gov.on.ca/fre/document/policy/admissions.pdf

www.edu.gov.on.ca/extra/fre/ppm/148.html

## Unayo maswali?

**Kwa taarifa zaidi, unaweza kuwasiliana na shule au bodi ya shule iliyo karibu zaidi kupitia katika www.elfontario.ca/fr/contacts.html**

## Inapatikana katika lugha 8 kwenye www.edu.gov.on.ca/fre/amenagement/

| English | Français | عربي | Kreyol | Español | Lingala | Kiswahili | Tiếng Việt |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| *Kiingereza* | *Kifaransa* | *Kiarabu* | *Kikrioli* | *Kihispaniola* | *Kilingala* | | *Kivietnamisi* |

ISBN 978-1-4606-2830-0 (PDF) ISBN 978-1-4606-2822-5 (Print) (Swahili)

Imechapishwa katika karatasi iliyotumiwa tena

© Kichapaji cha Queen cha Ontario, 2013